# AckySHINE.com

# TAFAKARI KUHUSU NAFASI YA MATESO NA SHIDA KATIKA MAISHA

By DIN - Melkisedeck Leon Shine · December 20, 2017

Makala za Tafakari Kwa Wakatoliki · Makala za Tafakari za Melkisedeck Leon Shine · #Karibu AckySHINE · #Tafakari za Myenendo ya Maisha · #Tafakari za Safari ya Kuelekea Utakatifu · #Tafakari za Toba na Msamaha

Ni kwa nini tunapata Mateso na shida katika Maisha? Kwa nini Mungu ameruhusu tuteseke?

Mungu hapendi mtu Ateseke lakini ni kwa njia ya ya Mateso mtu anaweza akapimwa IMANI yake, UNYENYEKEVU, UTII na Matumaini yake kwa Mungu.

Mateso na shida katika maisha ni nafasi ya kujifunza na Kuonyesha unyenyekevu, Imani na Matumaini ya mtu.

Mateso yanaweza kuwa malipizi ya dhambi kama adhabu au Majitoleo .

Mtu anaweza kujitesa au kukubali Mateso huku akiyachukulia kama malipizi ya dhambi zake au dhambi za wengine.

Sio rahisi kwa mtu wa kawaida kuweza kukubali au kujitesa kwa ajili ya dhambi hasa kwa dhambi zisizokua zake, Ni watu wachache Wenye fadhila hii. Mfano Watakatifu kama Mt. Faustina aliweza kuchukua Mateso kama malipizi ya dhambi hasa za watu wengine ambapo alikubali magonjwa shida na Kudharauliwa kama malipizi ya dhambi.

Yesu mwenyewe pamoja na Umumgu na Enzi yake alikubali Mateso kama Malipizi ya dhambi za watu na Kama njia ya Kuonyesha Unyenyekevu na Upendo.

Kumbuka, Mateso ni njia ya Kuonyesha unyenyekevu, Upendo na Kujitolea kwa hiyo ni kama malipizi na majitoleo hivyo sio lazima mtu ateseke au Ajitese ili aokolewe au aingie Mbinguni.

Mungu hapendi mtu ateseke ila anakubali Mateso kama njia ya kupima mtu na kumtakatifuza.

Mateso = Malipizi = Majitoleo = Kipimo cha Imani na Matumaini kwa Mungu

KUMBUKA: Ni kwa njia ya Mateso na Kifo cha Bwana wetu Yesu Kristo sisi tuliokolewa. Mababu wote Kwenye Biblia na Manabii walipitia dhiki na Mateso, Hata mitume nao waliteseka

Sio mara zote Mateso na Shida maana yake ni kuachwa na Mungu au Kuadhibiwa na Mungu, mara nyingine mateso ni majaribu, kipimo cha Imani na njia ya kujivika Utakatifu.

Mungu anakupenda sana, mtumainie yeye. Yote yanapita lakini yeye atasimama milele.

Mungu na Akubariki na kukupa Faraja.